

# MOLA WANGU NI ALLAH



سواحلي

maana na  
matunda ya  
kumuani  
Allwah na  
mitume yake

[www.with-allah.com](http://www.with-allah.com)



D. Muhammad bin sarrary Alyamaniy  
D. Abdullah ibn Saalim Bahamam

# Kumuamini Allah

Imani ya ukweli ni uhayi wa roho na ni uwanda wa furaha.



## KUMUAMINI Allah

### Maana ya kumuani Allah na hakika yake.

Imani ya ukweli ni uhai wa roho na ni uwanda wa furaha.

Raha ya nafsi haiji ila kwa kumuamini Allah, nafsi isio kuamini itabaki kuwa na kicho na niyenye kuduwala na dhaifu haina utulivu. Na imani ambayo ina kuokoka ni kumuani MwenyeEzzi Mungu, na maana yake ni kusadiki kwa kukatikiwa kwamba MwenyeEzzi Mungu ni Mola wa kila kitu, na nimfalme wake na muumbaji wake, na kwamba yeye anastahiki peke yake aabudiwe peke yake kwa swala kwa saumu kwa dua na kutarajiwa na kuogopwa na kumdhalilikia na kumnyenyekea, na kwamba yeye ndie mwenye kusifika na sifa za utukufu zote, mwenye kutakaswa na kila upungufu na kombo, mtukufu mshindi.

Na kumuamini MwenyeEzzi Mungu inakusanya kuamini malaika na vitabu vyake na mitume yake na siku ya mwisho na kuamni kadari kheri na shari yake, na imani ndio asli ya kusuudika mwanadamu , bali ndio pepo ya ulimwenguni kwa mumin, na mwisho wake ni pepo ya akhera insha Allah.

Na imani katika sharia ni kuamni kwa moyo na kutaamka kwa ulimi pamoja..

Na likijulikana hili, nalijulikane kwamba msingi wakukubaliwa amali kwa MwenyeEzzi Mungu ni kuamini, kwakusema kwake MwenyeEzzi Mungu (S.W): {Yoyote mwenye kufanya mambo mema na akawa ni mwenye imani}} (Al-anbiyaa 94)

Kumuamini Allah ni nuru ya uadilifu, na nuru ya uhuru, na nuru ya elimu na maarifaa, na nuru ya uongofu, na nuru ya utulivu na amani ya kiroho.

## Umuhimu wa imani

Hakika a'amali bora mbele ya Allah na tukufu zaidi ni imani, kwa hadiith iliyo pokewa na Abuudhari (R.A.A.) alipo muuliza Mtume (S.A.W) Ewe Mtume wa Allah niipi amali bora? akasema ni kumuamini Allah na kupigania dini yake. (Imepokewa na Muslim)

Nayo ni sababu ya uongofu na furaha ya dunia na akhera kwaneno lake Allah Mtukufu. {Basi yoyote ambaye Mwenyezi Mungu ataka kumuongoza huukundua moyo wake} (Al an-am : 125)

Na pia imani inamueka mbali muumini na maasi, kasema Allah aliyetukuka: {Walio muogopa MwenyeEzzi Mungu kikiwashika chochote cha shetani hukumbuka mara huwa wamekuwa waangavu.} (Al aaraf :201)

Imani ni sharti ya kukubaliwa a'amali ,amesema Allah Mtukufu



{Hakika umeletewa wahyi wewe na walio kuja kabla yako kwamba ukimshirikisha MwenyeEzzi Mungu itapomoka a'amali yako na hakika utakuwa miongoni walio pata hasara.} (Az-zumar 65)

Basi imani safi MwenyeEzzi Mungu huibariki na hutakabali kwa imani hiyo dua.

## MATUNDA YA IMANI

Anasema Allah Mtukufu {Huoni MwenyeEzzi Mungu alivopiga mfano wa neno zuri ni kama mti ulio mzuri asli imejik'ita ardhini na utanzu wake uku mbinguni, hutowa vyakula vyake kila mara kwa idhni ya Mola wake.} (Ibrahim : 24-25)

Na miongoni mwa matunda ya imani ni kama yafuatavyo:

1. Imani ya kweli hutia utulivu na raha ya nafsi na ukunjufu wa kifua. Na hili linasadikisha neno lake MwenyeEzzi Mungu

{Juwa kwamba wa penzi wa MwenyeEzzi Mungu hawana kicho wala hawatahuzinika } (Yunus 62)


2. Ni kupata waumini upamoja makhsusi kutoka wa MwenyeEzzi Mungu , yaani huwatoa kwenye giza ka ukafiri na shida zake kuwapeleka kwenye nuru ya imani na thawabu zake

3. Kufaulu kwa kupata radhi za Allah na pepo yake aliyo waandalilia waumini wake wakikweli kweli . kasema Allah Mtukufu: {Mwenyezi Mungu amewaahidi wanaomuamini wanaume na wanawake (amewaahidi) mabustani (pepo) zipitazo mito mbele yake kukaa humo daima, na makazi mazuri katika mabustani hayo yenye kudumu, Na radhi za Mwenyezi Mungu ni kubwa zaidi.} (At-tawba : 72)

4. Allah anawahifadhi na kuwakinga vipenzi vyake. {hakika mwenyezi mungu huwatetea walio muaamini } (Al-hajj : 38)

Miongoni mwahayo : Allah kumkinga Mtume wake Muhammad (S.A.W) katika tukio la kuhama kwake na jinsi Allah alimuhifadhi Ibrahim (A.W) alipotupwa ndani ya moto.

5. Utukufu katika dini na uongozi kwenye hiyo dini, amesema MwenyeEzzi Mungu (S.W): {Natukawafanya miongoni mwao maimamu wanaoongoza kwa amri yetu walipo subiri} (As-sajda 24)



**K u m u a m i n i**  
Allah ni  
u h u s i a n o  
baina ya mja  
dhaifu na mola  
wake , kama  
vile mwenye  
nguvu naye pia  
umuomba Allah.



<https://www.with-allah.com/sw>

Hakuna dalili kubwa ya hilo kuliko, utawala wa watu wa dini na yaqini juu ya Allah, Allah ameeendleza matukufu yao na wao wako chini ya matabaka ya michanga, miili yao imekosekana lakini athari zao na habari zao ziko kwenye maisha.

6. Mapenzi ya Allah kwa waumini , amesema Allah: {Mwenyezi Mungu anawapenda nao wanampenda} (Al-maaida: 54)

Na amesema Allah Mtukufu: {Hakika wale walioamini na kufanya a'amali mzuri (Mwenyezi Mungu ) atawapa upendo } (Maryam : 96)

7. Maisha mazuri ya dunia na akhera, Allah M t u k u f u a m e s e m a : { Y o y o t e m w e n y e k u f a n y a m e m a , a w e m u m e a u m k e , n a h a l i y e y e n i m w e n y e i m a n i t u t a m p a m a i s h a m a z u r i

**Uhayi pasina imani ni mauti yasiyo shaka.. mboni pasina imani ni up'ofu. Ulimi bila imani ni ububu. Mkono bila imani ni mlemavu.**

na tutawajazi malipo yao kwa vyema kuliko walivo fanya. } (An nahl 97)

Basi wako wapi wenye kutafuta maisha mazuri na furaha?

8. Mapenzi ya Allah kwa muumin na mapenzi ya muumin kwa Allah, anasema Allah: {Mwenyezi Mungu anawapenda nao wanampenda} (Al maaida 54)

Yaani anawapenda na anawawekea mahaba kwa watu .

9. Kupata bishara nzuri kwa watu wa imani kwa ukarimu wa Allah kwao .Allah Mtukufu asema: {wabashirie waumini } (At tawbah : 112)

Wala hakutolewi bishara illa kwa jambo kubwa, athari yake ikadhihiri juu ya ngozi ndipo ikaitwa bishara wala hakuna kikubwa kuliko rehma ya MwenyeEzzi Mungu na radhi zake na pepo yake, anasema Allah: {Wabashirie walioamini na wakafanya mema kwamba wana mabustani yanayo pita chini } (Al baqarah 25)

10. Imani ni sababu ya kuthubutu, anasema Allah Mtukufu: {Wale ambao watu (waliwatisha) Wakawaambia, watu Wamewakusanyia, waogopeni (hilo) likawazidishia imani na wakasema tosho letu ni MwenyeEzzi mungu alie mwema wakutegemewa } (Aal imran 173)

Wala hakuna ambalo ni dalili kubwa ya kuthubutu huku kuliko yale yaliyo



andikwa na tarikhi kuhusu mitume na maswahaba na waliofuatia wao, na alie kwenda juu ya mwendo wao.

11. Kufaidika na mawaidha, anasema Allah Mtukufu: {Basi wakumbushe, kukumbusha kunawafaa waumini } (Adhariyat : 55)

Hawafaidiki na mawaidha ila watu wa imani

12. Amiweka kheri kwa hali zote kwa mwenye imani, katika hali ya furaha na katika hali ya dhiki, kheri huwa ni yenye kuambatana na muumin. Ni ajabu mambo ya muumin hali zake zote kwake ni kheri halipatikani hili ila kwa muumini, akipata mazuri hushukuru ikawa kheri kwake, na yakimsibu madhara husubiri ikawa kheri kwake. (Imepokewa na Muslim)

Kwahiyo imani inampeleka mtu kuwa na subra wakati wa madhara, na kushukuru wakati wa mapesi.

13. Kuhifadhiwa muumin na kuingia katika madhambi makubwa, limeswihi neno lake: Mtume (S.A.W) "Hazini mwenye kuzini ila huwa hana imani wakati huo" (Imepokewa na Bukhari)

Haya ni matunda mema ya ubora wa imani, basi wako wapi wenye kutafuta kusuudika na raha ya moyo na utulivu



## ATHARI ZA IMANI

Miongoni mwa athari  
za imani kwa maisha ya  
muumin:

1. Kuongezeka pupa ya muumin katika kufuata sharia tukufu , asema Allah Mtukufu {Haiwi kauli ya waislamu wanapoitwa kwa mwenyezi mungu na mtume wake ili ahukumu baina yao,ila husema :“tumesikia na tumekubali,”na hao ndio wenye kufaulu } (An-nur 51)

Basi imani humpeleka mwenye nayo kwenye kufanya haraka kufuata na kunyokea amri ya MwenyeEzzi Mungu.

**Kumuamini  
Allah ni  
uhayi ..na  
u h a y i  
pamoja na  
Mungu ni  
kuamini.**

Asema Allah Mtukufu {Basi sio naapa kwa Mola wako hawatoamini mpaka wakufanye wewe ndie hakimu wao kwenye utesi uliozuka kati yao kisha wasipate katika nyoyo zao shida kwa ulilohukumu na wajisalimishe kabisaa. } (An-nisaa : 65)

Bali imani inampeleka muumin kusalimu amri na kuridhia na amri za Allah mtukufu.

2. humuhifadhi MwenyeEzzi Mungu mja wake na shirki wazi na ilojificha , na nikatika hayo: kutopeleka cha maombi chochote au chakutaka msaada au kutaka kuokolewa popote kwa asie kuwa MwenyeEzzi Mungu, mwenye kunufaisha na mwenye kudhuru ni Allah: {Na Akikugusa MwenyeEzzi mungu kwa madhara yoyote hakuna mwenye kuyaondoa asie kuwa yeye } (Al-an-am 17)

3. Kupenda na kuchukia kuwe kwa ajili ya Allah , na hiyo ndiyo kamba imara mno ya imani , anasema Allah Mtukufu: {Hakika waumini ni ndugu } (A-lhujuraat :10)

Wala hakuna dalili kubwa kwa hilo kuliko kuwafanya ansari na muhajirina ni ndugu, na kujitolea kwao nafsi zao na malo yao kuwapa ndugu zao, alisema mtume (S.A.W) “Hatuumini mmoja wenu mpaka ampendele nduguye analo jipendelea.” (Amepokea Bukhari)



4. Kusubiri kwenye jihadi kwa ajili ya MwenyeEzzi Mungu na kutoa vilio ghali na vitukufu kwa ajili ya kumridhisha Allah, anasema mtukufu : {Hakika waumini tu ni wale walio muamini na mtume wake kisha wasifanye shaka na wakapigana jihadi kwa mali yao na nafsi zao katika njia ya Allah hao ndio wa kweli.} (Al-hujurat 15)

**{Enyi mlioamini aminini}.  
Aliwaita kwenye imani na  
kuwahimiza kwasababu ya  
ubora wake.**

5. Moyo kuambatana na Mungu na ahadi yake na kusuudika kwake kwa hilo, pepo ya ulimwengu kwake yeye ni kuamni na kumtii Allah, na ataraji pepo ya aakhera Ambayo ni ahadi ya MwenyeEzzi Mungu kwake, kamwe ataraji thawabu ya MwenyeEzzi mungu kwa kila limkumbalo katika shida na

tabu na usumbufu, na yaandikwe kwenye aamali zake, anasema Allah: {Haikuwa sawa kwa watu wa madina na walio pambizoni mwao miongoni mwa mebedui wabaki nyuma wasende na mtume, wala wajipendele wao kuliko kumpendelea yeye hilo ni kwakuwa haiwasibu wao kiu wala sumbuko wala shida katika njia ya MwenyeEzzi Mungu, wala hawakanyagi popote penye kuwatia hasira makafiri wala hawamtii adui utungu wowote isipokowa huandikiwa wao kwa hilo aamali njema wala MwenyeEzzi Mungu hapotezi malipo ya wenye kutenda wema. wala hawatoi chochote kidogo wala kingi wala hawakati wangwa (kwa safari) ila huandikiwa wao ili awalipe wao Mema mno, yayale wailokuwa wakiyafanya.} (At tawba 120-121)

Yote haya ni ya watu wa walio muamini Allah na wakamswadikisha katika matendo yao.

6. Kupata uwalii (URAFIKI) wa Allah na Mtume (s.a.w) Aesema Allah Mtukufu {Rafiki yenu khasa ( wakumsafia nia ) ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na waliomini ambao husimamisha sala na hutoa zaka, na hali yakuwa wananyenyekea.} (Al maidah 55)

Uwalii wa Allah ni: kumpenda Allah mtukufu na kunusuru dini yake na kuwapenda mawalii wake na kuwakata wote wasiokuwa hawa kwasababu ni maadui wa Allah Mtukufu.



Amesema Allah Mtukufu: {Huwapati (huwaoni) watu wanaomuamini MwenyEzzi Mungu na siku ya mwisho, kuwa wanawapenda wale wanaopinga MwenyEzzi Mungu na Mtume wake; hata wakiwa ni baba zao au watoto wao au ndugu zao au jamaa zao. Hao ndio ambao (mwenyEzzi mungu) ameandika (amethibitisha kweli kweli) nyoyoni mwao imani na atawaingiza katika mabustani yapitayo mito mbele yake; humo watakaa daima. Mwenyezi Mungu amekuwa radhi nao, na wao wamekuwa radhi naye. Hao ndio kundi la mwenyEzzi mungu ndilo linalofaulu.} (Al-mujadilaa 22)

Muumini anampenda Allah na Mtume wake na waumini wote na wala hawafanyi makafiri kuwa marafiki wake katu, asema Allah Mtukufu:

{Walioamini wasiwafanye makafiri kuwa wapenzi wao ( wa kuwapa siri zao) badala ya (waislamu wenziwao).} (Aali imran 28)

7-Kupata tabia nzuri, imethibiti kutoka kwa mtume ( s.a.w) Haya na imani yaenda pamoja, ikiondoka moja yapili nayo yaondoka. (Imepokewa na Baihaqi)

Na sifa ya haya ni miongoni mwa tabia nzuri muumini anajaribu kutengeza muamala wake na ndugu zake waislamu ili aishi katika neema za dunia bila mashaka wala chuki... yote haya kwasababu yeye ni muumin, hayapatikani haya ila kwa muumin.

Furaha ya hakika na raha halisi ya moyo, kiwango ambacho anahisi kuwa yuko peponi haliyakuwa yuko duniani kwa sababu ya raha anayo ihisi katika utulivu wa moyo, kwa sababu yuko na Allah Mmoja pekee na Mtume mmoja

ni Muhamad (s.a.w) na njia moja nayo ni kufuata radhi za Allah na lengo moja ni pepo iliyo na mapana kama mbingu na ardhi.

Hakika siku hizi unaona zahanati nyingi za ungonjwa wa nafsi kila mahali, zilizo jaa wagonjwa wa nafsi kila mtu analia kutopata utulivu wa moyo na wasiwasi na mstuko wa roho na kukosa usingizi, hapo ndipo ujuapo kwa yakini yote haya nisababu ya kuwambali kwao na imani ya Allah ya

uhakika wake, na sababu ya kuegemea dunia na kufungamana nayo sana, kwasababu kupenda vitu kumeingia ndani ya nyoyo zao. mwanadamu anahitaji sana kupata chakula cha moyo na haya hayawi ila kwakuamini imani ya haki na kushikana nayo na kudumu kuitaja na kuamini malaika na vitabu vitakatifu na mitume na kuamini siku ya mwisho na qadari nzuri au shida zote zatoka kwa Allah.

Lakuzingatia ni kuwa watu wengi wameghafilika na dawa ya moyo na utulivu wa moyo, na pepo ya dunia na wakaelekea nyuma ya mapato ya dunia isio dumu ndio maana haija wakamilishia waliyo yataka wala hawajawahi kupumzika tokea mwanzoni mwa njia.

Na kutosheleza matakwa ya moyo hayapatikani ila kwa imani, kwa sababu moyo zimetoka kwa Allah, na mwili aliwuumba Allah kutokana na mchanga, kila zitakapotosheka nyoyo kwa imani hupatikana heshima na utukufu na hutulia na hujiepusha na mambo yasiokuwa na faida, na kila likisahulika hili la kuitosheleza nafsi kwa imani, anakuwa mwanadamu kama mnyama mwenye kushindwa na matamano ya nafsi yake na kupata dhiki na unyonge .



# KUAMINI MITUME WA Allah WALIO MTANGAZA .

Hakuumba Allah waja wake bure tu bila sababu, na wala hakuwaacha bure, ndipo aliwatumia mitume wake ili wamtangaze Allah, na utukufu wake, na ukamilifu wake, na kutangaza sharia zake, na Allah ametuma katika kila watu mbora wao ,akatuma mitume mingi sana miongoni mwao: Nuh Ibrahim,Musa,Issa, (a.s) na mwisho akamtuma Mwisho wa manabii, Mbora wa viumbe wote Muhamad (s.a.w) na akawapatia kila Mmoja miujiza yake yenye kujulisha ukweli wao, wakafikisha amana, na wakatekeleza jukumu la utume, na wakawafahamisha waja kuhusu Mola wao na muumba wao, basi asie amini risala yao na kutokubali hajamuamini Allah. Amesema Allah. {Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa mola wake, na waislamu,( pia wameamini hayo ):wote wamemwamini Mwenyezi Mungu, na malaika wake na vitabu vyake, na mitume yake} (Al baqarah 285)

Kwasababu wao ndio walio tufikishia ujumbe wa Allah mtukufu kwahiyo tunawaamini wote. Allah amesema: {Hatutafautishi baina ya yoyote katika mitume yake (wote tunawaamini) } (Al baqarah 285)

Allah Mtukufu ametuma hawa mitume pamoja na vitabu ili viwe nuru kwa wanadamu, akatuma pamoja na nabii Ibrahim sahifa na pamoja na nabii Daudi zabuur na pamoja na nabii na Musa taurat, na pamoja na nabii Issa injil na pamoja na Mtume Muhamad (s.a.w) quran kitabu kilicho na miujiza {Hiki ni kitabu ambacho aya zake zimetengenezwa vizuri, kisha zikapambanuliwa (vyema) kutoka kwa (Mwenyezi Mungu)Mwenye hikima na Mwenye ujuzi wa kila kitu." (Hud 1)

Amekifanya Allah kuwa ni uongofu na nuru na baraka na dalili. asema Allah Mtukufu: {Na hii qurani ni kitabu tulichokiteremsha (kwenu), kilicho na baraka nyingi. basi kifuateni na muwe wacha mungu ili mrehemewe} (Alan-am 155)

Na akasema tena: {Enyi watu! Imekufikieni dalili kutoka kwaa mola wenu, na tumekuteremshieni nuru iliyo dhahiri.} (An nisaa 174)

Allah amejalia kuamini Mtume Muhamad (s.a.w.) na kuamini ujumbe wake kuwa pamoja na kumuamini yeye pekee, katika kalma ya shahada ambayo ni kushuhudia kuwa hakuna apaswaye kuabudiwa kwa haki illa

Allah, na kushuhudia kuwa Muhamad (s.a.w) ni Mtume wake, amemtuma Allah Mtukufu kuwa rehema ya walimwengu, akawatoa kutoka giza paka kwenye nuru, na kutoka kwa ujahili paka kwa elimu na kutoka kwa upotevu paka kwenye uongofu, akafikisha amana na akawanasishi watu na alikuwa na pupa juu ya umma wake.

Amesema Allah Mtukufu: {Amekufikieni mtume aliye jinsi moja na nyinyi, yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni. (na) kwa walioamini ni mpole na mwenye huruma} *At tawba 128*

Allah akampa Mtume wake miongoni mwa haki anazostahiki, yeye ni mbora wa viumbe vyote na bwana wao, asema Mtume (s.a.w) *Mimi ni bwana wa watoto wa Adam wala sikujisifu. (Imepokewa na ibn maja)*

Na miongoni mwa haki zake :

1. Kuamini yeye ni mja wa Allah na Mtume wake na Allah amemtuma kuwa rehema kwa waja wake, na alifikisha amana, na akatekeleza risala , asema Allah mtukufu: {Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na nuru tuliyoiteremsha,(qur'an)} *(Taghaabun 8)*

Amesema mtume (S.A.W) "Naapa na Yule ambaye nafsi ya Muhamad iko mikononi mwake hakuna atakaye sikia ujumbe wangu huu miongoni mwa watu wa uma huu awe yahudi au mkristo kisha afe bila kuamini niliyo kuja nayo ispokuwa atakuwa ni mtu wa motoni " *(Imepokewa na Muslim)*

2. Kukubali na kusadikisha aliyokuja nayo kutoka kwa Mola wake Mtukufu na kuyakinisha kwamba ni haki kutoka kwa Allah Mtukufu bila shaka. Asema Allah Mtukufu: {Wenye kuamini kweli kweli ni wale waliomuamini mwenyezi mungu na mtume wake kisha wakawa si wenye shaka} *(Al-hujurat 15)*

Amesema Allah Mtukufu: {Naapa kwa Mola wako, wao hawawi wenye kuamini (kweli kweli) mpaka wakufanye (wewe ndiye) hakimumu (mwamuzi) katika yale wanayokhatalifiana, kisha wasione uzito nyoni mwao juu ya hukumu uliyotoa, na wanyenyekee kabisa} *(An nisaa 65)*

3. Kumpenda Mtume(S.A.W) asema Allah Mtukufu {Sema:"kama baba zenu na wana wenu na ndugu zenu na wake zenu na jamaa zenu na mali mlizochuma na biashara mnazoogopa kuharibikiwa, na majumba mnayoyapenda;(ikiwa vitu hivi ) ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na mtume wake na kupigania dini yake,basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake; na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu maasi } *(At tawbah 24)*

Na akasema Mtume (S.A.W) "Haja amini mmoja wenu paka niwe kipenzi chake zaidi ya wazazi wake na watoto wake na watu wote" (Imepokewa na Bukhar)

4. Kumuheshimu na kumtukuza Allah , amesema Allah: {Ili mumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mumsaidie, na mumhishimu, na mumtakase asubuhi na jioni.} (AL-FAT-H 9)

Na akasema tena: {Basi wale waliomuamini yeye na kumuheshimu na kumsaidia na kuifuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye (quran) hao ndio wenye kufaulu} (Al aaraf 157)

5. Kupenda na kuwatukuza ahli baiti watu wanyumba yake walio silimu na wakafuata njia yake, na kufahamu wasia wa mtume wetu Muhamad (s.a.w) amesema : Nawakumbusha kwaajili ya Allah kwa watu wanyumbani kwangu na wakumbusha kwaajili ya Allah kwa watu wanyumbani kwangu. (Imepokewa na Muslim)

Na watu wanyumbani kwa mtume (s.a.w) ni wale masharifu, kama: wakeze mtume (s.a.w) na watoto wake na jamaa zake wakaribu, walio haramishiwa kuchukua sadaka haifai kuwatweza wala kuwatukana kama vile haifai kudai kuwa hawafanyi madhambi wala kuwaomba kinyume na Allah.

6. Kupenda maswahaba wake walio muamini na wakamsadikisha bila kuwataja kwa ubaya kwani Allah amewasifu katika kitabu chake.



7. Haifai kuwasema maswahaba wake kwa ubaya wale waliomsadikisha na kumuamini nao ni aliowasifu Allah katika kitabu chake aliposema: {Muhamad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na waliopamoja naye ni wenye nyoyo thabiti mbele ya makifiri na wenye kuhurumina wao kwa wao. utawaona wakiinama kwa kurukuu na kusujudu (pamoja), wakitafuta fadhila za mwenyezi mungu na radhi zake alama zao zi katika nyuso zao kwa taathira,(athari)ya kusujudu} (Al fathu :29)

Na akasema Mtume(s.a.w) kuwahuu: Msiwatukane maswahaba wangu, msiwatukane maswahaba wangu, naapa na Yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake kama mmoja wenu atatoa mfano wa dhahabu kiwango cha mlima uhud hawezi kufika kibaba cha thawabu zao wala nusu yake (Imepokewa na Muslim)

Na maswahaba bora zaidi ni makhalifa wanne walioongoka; Abubakar na Umari na Uthmani na Alii (r.a) amesema Allah Mtukufu. {Na wale waliotangulia wakawa wa kwanza katika(uislamu)-muhajirina na answari, na wale waliowafuata kwa mwendo mzuri – mwenyezi mungu atawapa radhi, nao wamridhie (mwenyezi mungu kwa hayo mazuri atakayowapa) na amewaandalia mabustani yapitayo mito mbele yake, wakakae humo milele. huku ndiko kufuzu kukubwa.} (At tawba 100)

Wote hawa walifikisha walioyapokea kutoka kwa Mtume (s.a.w) mpaka ikatufikia nasi elimu ya dini.

## Kuamini kukutana na Allah

Kila kiumbe kitarudi kwa Allah na kwake ndio marejeo ya kila kitu, na hii ni nguzo muhimu sana katika nguzo za imani, miongoni mwa nguzo za imani kuamini siku ya mwisho imethibiti kuwa Mtume (s.a.w) alipoulizwa na Jibril (a,s) mbele ya maswahaba kutaka kuwafundisha nguzo za imani. akasema . **“Ni kuamini Allah na malaika wake na vitabu vyake na mitume wake na siku ya mwisho na kuamini qadari kheri na shari yote yatoka kwa Allah.”** (Imepokewa na Muslim)

Na imeitwa siku ya mwisho kwasababu hakuna siku baada yake watakapo kuwa watu wapeponi peponi na watu wa motoni motoni. na iko na majina mengi katika quran tukufu inayojulisha utukufu wake na ukubwa wake na yatakayo tokea siku hiyo:

Siku ya kutokea jambo kwasababu siku hiyo itatokea , na khafidha yenye kutweza na kunyenyua kwasababu watanyenyuliwa watu darja peponi na watatweza wengine motoni, siku ya hisabu na malipo, na siku ya dini na siku ya haki ambayo khabari zake Allah zitakuwa kweli, siku ya balaa na siku ya sauti kali iumizayo mashikio, kwasababu mpulizo wa baragumu unaleta uziwi, na siku na ahadi, kwakutimia ahadi zake Allah juu ya makafiri, na siku ya hasara, kwa hasara na majuto, na siku ya kukutana, kwasababu watu wote watakutana sehemu moja, na siku iliyo karibu kwa ukaribu wake, siku ya kuitana, kwasababu ya watu kuitana watu wa peponi watawaita watu wa motoni na watu wa motoni wawaite watu wa peponi na siku tasa siku ya mwisho hakuna siku baada yake na nyumba ya mwisho na nyumba ya milele na siku ya kufinika kwa sababu itafinika watu na majina mengine .





## **YANAYO AMBATANA NA IMANI YA SIKU YA MWISHO.**

**Mwanzo: Kuamini ya  
baada ya mauti**

**Kama fitna ya kaburini .**

Nayo ni kuulizwa maaiti baada yakuzikwa kuhusu mola wake na dini yake na nabiyi wake, hapo huwathubutisha Allah kwa neni la kuthubutu wale ambao wameamini, akaseama: ( Mola wangu ni Allah, na dini yangu ni uislamu, na mtume wangu ni Muhammad), na huwapoteza Allah walio madhalimu hapo husema alio kafiri:(ha..ha.. sijui), na husema mnafiki au mwenye shaka:(sijui nimesikia watu wakisema kitu nami nikasema).

**Na miongoni mwa adhabu za  
kabri na neema zake**

Adhabu ya ya kaburi huwa ni yamadhalimu na manafiki na makafiri,na baadhi ya maasi miongoni ya waumini.amesema Allah mutukufu: {Na lau ungewaona madhalimu kwenye matungu ya mauti na malaika wamenyosha mikono yao toeni roho zenu leo mtalipwa adhabu ya utwevu kwa yale mulikuwa mukiyasema kwa Mungu yasiokuwa ya haki na mulikuwa mukifanya kibri kwa aaya zake } (Al-an'am 93)

Allah amesema Mtukufu kuhusu watu wa Firaun {Watakuwa wakionyeshwa asubuhi na jioni na siku itakapo simama kiyama (kutaambiwa)watiyeni watu wa firauni kwenye adhabu}} (Ghaafir 46)



Na katika hadith ya Zaid bin Thabit kutoka kwa mtume ( s.a .w) "Lau Kama haingekuwa hamtazikana , ningemuomba Allah akawasikizisha baadhai ya adhabu ya kaburi ambayo naisikia, kisha akatuelekea kwa uso wake, akasema : twajilinda kwa mweneEzzi Mungu na adhabu ya kaburi, tukasema: twajilinda kwa Allah na adhabu ya kaburi, akasema: twajilinda kwa Allah na adhabu ya kaburi, akasema: twajilinda kwa Allah na adhabu ya kaburi, akasema twajilinda kwa Allah na fitna zilizodhihiri na zilizojificha,tukasema twajilinda kwa Allah na fitna zilizodhihiri na zilizojificha,akasema twajilinda kwa Allah na fitna za Dajaali " (Amepokea Muslim)

Ama neema za kaburini niza waumini wa kweli, amesema Allah mtukufu: {Hakika Wale ambao walisema Mola wetu ni Allah kisha wakalingana sawasawa wanawateremkia malaika (kuwaambia), "kwamba musiche wala musihuzunike na furahikieni pepo ambayo mlikuwa.} (Fusilat: 30)

Na Amesema Allah Mtukufu: {Basi roho itakapofika k'oni. na nyinyi hapo

mwatizama .nasi tukokaribu nayo kuliko nyinyi lakini hamuoni. Basi laukamahamutalipwamungeirudisha hiyo roho ikisafika k'oni mungekuwa wa kweli. Ama akiwa mwenye kufa ni miongoni waliokurubishwa na Allah. Atakuwa na raha na riziki njema. Ama akiwa katika watu wa upande wa kulia. salama ni yako kwakuwa ni katika watu wa kulia.ama akiwa katika wenye kukanusha walio wapotevu. basi wana mashukio ya moto wa jahanam.na kuchomwa katika moto wa jaihim.hakika huu ndio ukweli wa yakini. Basi litukuze jina la Mola wako mtukufu } (Al-waqiah 83- 96)

Na amesema kuhusu mwenye kuamini akiwajibu malaika wa wili katika kabri yake Ataita mwenye kuita kutoka mbinguni kwamba amesema kweli mja wangu, mtandikieni peponi,na mumvalishe kutoka peponi, na mumfungulie mlango wa peponi, akasema hapo yatamjilia manukato yake,na atafungulwa kaburini mwake upeo wa macho yake". (Ahmed, abu dawud, katika hadeeth ndefu)



## Pili: kuamini kufufuliwa.

Nako ni kuwuhiyiwa watu kutakapo viviwa parapanda viviwa la pili, watu watasimama kwa ajili ya Mola wa viumbe wote, hali yakuwa bila ya viyatu, wakiwa uchi bila yakujisitiri, wakiwa mizunga bila yakutahiriwa, amesema Allah: {Kama tulivoanza kuumba tutakuregesha ni ahadi juu yetu hakika sisi ni wenye kulifanya hilo)} (Al-anbiyaaa 104)

Na kufufuliwa ni haki yenye kuthubutu ilio onyeshwa na qur'an na sunnah na kongamano la waislamu, amesema Allah mtukufu: {Kisha nyinyi baada ya hapo mutakufa . kasha nyinyi siku ya kiyama mutafufuliwa.} (Al-mu'minun: 15-16)

Amesema Mtume (s.a.w) Watafufuliwa watu siku ya kiyama bila ya viatu na mazunga" (Mutafaqu alaihi)

Na wamekongamana waislamu kwa kuthubutu kwake, na hilo ndilo la hikma linalotaka mwenyeEzzi Mungu avaveke hawa viumbe maregelewa watakapolipwa yale waliolazimishwa kwa ndimi za mitume wao. Amesema Allah mtukufu: {Mwadhanja kwamba tumewaumba to na kwamba hamutarudi kwetu ?} (Al-muminun 115)

Na MwenyeEzzi Mungu amewaambia mitume: {Hakika MwenyeEzzi Mungu ambae amekufaradhia qur'an ni mwenye kukuregesha kwenye maregewa.} (Al-qasas 85)

Alikuwa Uthman akisimama juu ya kaburini hulia mpaka akarowesha ndevu zake akasema: akaambiwa: kwatajwa pepo na moto hulii, na walia kwa hili? Kasema: hakika mtume wa MwenyeEzzi Mungu alisema: "hakika kaburi ni mashukio ya kwanza katika mashukio ya akhera, akiokoka nayo litkalo kuja baada yake ni rahisi, na akitookaka nayo yaliyo baada yake ni magumu zaidi" akasema: na akasema: sikuona cha kuangaliwa ila kaburi yatisha zaidi". (Ameipokea Ahmed)




## Tatu : kuamini yaliyo kuja kuhusu alama na ishara za siku ya kiyama:.

Nazo nizile zitakazo tangulia kuja kiyama chenyewe na zenye kuonyesha ukaribu wa kuja kwake, na kumezoewa kuzigawanya hizo alama mara mbili alama za ishara ndogo na alama za ishara kubwa.


### ALAMA NDOGO

Nazo nizenye kutangulia siku ya kiyama-mara nyingi- kwa muda mrefu , na miongoni mwazo kuna zilizitokea na zikamalizika- na henda zikakaririka – (kuja mara kwa mara) na kuna zilizo jitokeza na zikaendelea kujitokeza , na kuna ambazo hazijatoka mpaka sasa, lakini zitatoka kama alivosema mkweli mwenye kusadikiwa-, kama: kutumilizwa mtume na kufa kwake, na kufunguliwa betul-makdisi, na kudhihiri fitna, na kupotea uwaminifu, na kupotea ilmu na kudhihiri ujinga, na kuenea zina na riba, na kudhihiri aala za nyimbo, na kuzidi kunywewa mvinyo, na kutukuka wachunga mbuzi kwenye majumba, na kuzidi kuteta watoto na wazazi wao mpaka wajifanye kama kwamba wao ni mabawana zao, na kuzidi kuwa na mitetemeko ya ardhi, na kudhihiri kudidimizwa na kugeuzwa na kutukananwa, na kudhihiri wanawake walio vaa wenye kuenda uchi, na kuengezeka kutolewa ushahidi wa urongo na kufichwa ushahidi wa ukweli, na mengi yasio kuwa hayo miongoni yalio kuja katika kitabu cha Allah na sunna za mtume.



## Alama kubwa:

Nazo ni mambo makubwa kutaonyesha kuja kwayo kukurubia kuja kiyama na kubaki mda mfupi wa kuja hiyo siku kubwa, nazo ni alama kumi: Djali, na kuteremka lysaa mwana wa mariyamu, na Yajuja na Majuja, na kupatwa mwezi mara tatu: kupatwa mashariki, na kupatwa magharibi, na kupatwa kwenye kisiwa cha kiarabu, na moshi, na kutoka jua magharibi, na mnyama, na moto ambao utawapeleka wato kwenye kufufuliwa kwao, na alama hizi zitatokeza kwa kufuatana, ikidhihiri ya kwanza ya pili ya fuatia.



## Nne : kuamini yaliyo kuja kuhusu vituko vya kiyama na matukio yake kama:

1. Kusagwasagwa majabali na kufanywa mchanga yawe sawa na ardhi.

amesema Allah mtukufu {Na utayaona majabali utayadhania yametulia nayo yakimbia yanavo kimbia mawingu.} (An-namli 88)

Na akasema Allah Mtukufu {Na yatajunjavunjwa majabali yawe vumbi lilo t'atawanywa } (Waqiah aya 6-7)

Amesema Allah Mtukufu {Na milima itakuwa kama sufi (inayoruka)} (Ma,arij aya 9)

Na amesema Allah Mtukufu: {Na wanakuuliza kuhusu majabali sema atayavunjavunja Allah kabisa. Atayawacha kiwanda kilicho tandikwa. Hayana uchini wa ukubwa. } (Ta ha aya 105-107)

2. Kulepuka bahari na kutiwa moto, hizi bahari zenye kufinika sehemu nyingi ya ardhi yetu, zitalepuliwa siku hiyo, amesema Allah mtukufu: {Nabahari zitakapolipuliwa } (Infitar aya 3) {Na bahari zitakapowashwa moto} (Takwiyar aya 6)

3. Kubadilika ardhi hii wanayo ijuwa watu, na vilevile mbingu, wafufuliwe juu ya ardhi wasiojuwa , amesema Allah mtukufu {(Siku itakapobadilishwa ardhi iwe sio hii ardhi na zibadilishwe mbingu na watokeze kwa MwenyeEzzi Mungu m'moja mwenye kushinda nguvu. .} (Ibrahim aya 48)

Akasema Mtume (s.a.w) " watafufuliwa watu siku ya kiyama juu ya ardhi nyeupe yenye kupigia wek'undu kama donge la unga haina alama ya yoyote . (Mutafakun alyhi)

Itakuwa nyeupe bila alama yoyote

4. Wataona watu Wasilokulizowea kwani wataona kukutana jua na mwezi, roho zitazidi kukereka na kubabaika, amesema Allah mtukufu {(Itakapo duwala jicho. Na mwezi ukazima mwangaza wake. Na kukakusanywa jua na mwezi. Atasema mwanadamu siku hiyo pakukimbilia ni wapi? } (Qiyamah aya 7:10)





5. Kupulizwa parapanda na ndiko kukoma maisha haya ya ulimwenguni, itakapokuja siku hiyo kutapulizwa parapanda, kupulizwa huku kutakomesha maisha haya ya ulimwenguni. {Na kutapulizwa parapanda(baragumu) wasusuwikwe walio mbinguni na ardhini ila alio wataka MwenyeEzzi Mungu (wasiwe hivo)}} (Az-zumar aya 68)

Nako ni kupulizwa kukubwa kwenye kuharibu kila kitu, atakokokusikia mtu na asiweze kufanya lolote , nawala asiweze kurudi kwa watu wake na marafaki wake. {Hawangojei ila ukelele mmoja tu utakao kuwashika kwenye hali yakuwa wanagombana . hawatoweza kutoa wasia nawala hawatorudi kwa watu wao.. (Ya-sin aya 49-50)

Asema mtume (s.a.w) {Kisha kutapulizwa baragumu hatulisikia yoyote ila ataipendua na ainue shingo yake, akasema- (mtume)na wakwanza kusikia hayo ni mtu atakaakuwa analitengeza birika la ngamia wake,akasema(mtume) atasusuwikwa(kuanguka na kupoteza fahamu)na watasusuwikwa watu ."} (Imepokewa na Muslim)

6. Kufufuliwa na kukusanywa kwa viumbe wote tangu alipo viumba Allah paka siku ya kukusanywa ,watakusanyika Katika uwanja huo tangu wamwanzo wao mpaka wamwisho wao majini na watu, pia wanyama, amesema Allah {Kwa yakini katika haya kuna mazingatio kwa yule anayeogopa adhabu ya akhera.hiyo ndiyo siku itakayokusanyiwa watu, na hiyo ndiyo Siku itakayo shuhudiwa(na viumbe wote) } (Hud aya 103)

Asema Allah Mtukufu {Sema, "bila shaka wa kwanza na wa mwisho" "watakusanywa kwa wakati (uliowekwa) katika siku maalumu."} (Waqiah 49:50)

7. Hakika watu watafufuliwa wakiwa uchi kama walivyo umbwa na Allah wala hawatapepesa kushughulika na hilo kwasababu ya ugumu wa sehemu hiyo na kisimamo hicho chenye kutisha, hapo alishangaa mama Aisha (r.a) akasema kama anavyo simulia mwenyewe Alisema Mtume wa Allah (mtafufuliwa hali mkiwa uchi hamja tahiriwa),akasema aisha (r.a) nikasema ewe mtume wa Allah wanaume kwa wanawake wakiangaliana? akasema jambo ni gumu zaidi kuliko kushughulika na hayo" (Imepokewa na Bukhari )

8. Kulipiza kisasi kwa mwenye kudhulumiwa hata wanyama nao watalipizana visasi asema Mtume wa Allah (s.a.w): **Hakika mtarudisha haki zawatu siku ya kياما paka ataletwa mbuzi asiye na pembe amlipize aliye nazo ambaye alimdonga duniani.** (Imepokewa na Muslim)

Na akasema tena (s.a.w) **"Ambaye alimdhulumu nduguye muislamu kwa cheo chake au kwa kitu chochote basi ajivue nacho hapa ulimwenguni kabla ya siku ya kياما ambapo hazitafaa pesa bali kama ana vitendo vizuri vitachukuliwa kulingana na madeni anayo daiwa na kama hana vitendo vyema yatachukuliwa maovu ya wenye kudai na arundukiziwa yeye."** (Imepokewa na Bukhari)

9. Jua kushuka karibu na watu, mpaka watu wafinikwe na majasho yao kulingana na vitendo vyao amesema Mtume wa Allah (s.a.w) **"Jua litashushwa karibu siku ya kياما mpaka liwe karibu na viumbe kadri ya mail moja, akasema Suleim bin Amri:"** naapa kwa Allah sijui alikusudia nini mail moja? sijui ni masafa ya ardhi au ni kijiti cha kupakia wanja ? akasema watu watakuwa katika majasho yao kadri ya matendo yao, kunaye ambaye jasho litafika visiginoni mwao na kunao yatafika magotini mwao na kunao yatafika shingoni mwao na kunao yatawafinika majasho yao akaashiria Mtume (s.a.w) kwa

**mkono wake mdomoni mwake."**  
(Imepokewa na Muslim)

10. Kunaye atachukua kitabu chake kwa mkono wa kulia, na kunaye atachukua kwa mkono wa kushoto kisha watu watakuwa na wasiwasi na uoga paka daftari lake liwe mkononi mwake hapo ndio muumin atafurahi kwakuridhia kufaulu pindi atakapo shika daftari lake, ilhali makafiri na wanafiki wanaongezeka majonzi na wasiwasi pindi watapo yakamata madaftari yao kwa mikono yao ya kushoto, hayo ni malipo yaliyo sawa, asema Allah Mtukufu {Basi ama yule atakayepewa daftari lake kwa mkono wake wa kiume (kulia) atasema (kwa faraha)" haya someni daftari langu (nililopewa sasa hivi). "Hakika nilijua ya kuwa nitapokea hisabu yangu (kwa vizuri, kwani nikifanya mazuri)" basi yeye atakuwa katika maisha ya raha .katika pepo tukufu. Vishada vya matunda yake vitakuwa karibu;(vinachumika bila ya taabu) (waambiwe): kuleni na mnywe kwa furaha kwa sababu ya vitendo mlivyofanya katika siku zilizopita. "Walakini atakayepewa daftari lake kwa mkono wake wa kushoto basi yeye atasema. "Ooh laiti nisingalipewa daftari langu."Wala nisingalijua ninini hisabu yangu." Laiti (mauti )yangemaliza (kila kitu changu)"mali yangu haikunifaa ."Usultani (ukubwa) wangu umenipoteta.} (Alhaqqah 19-29)



11. Yatayomsibu mtu katika hofu na uoga kiwango mtu hawezi kumuuliza mwingine lolote halimshughulishi ila nafsi yake anasema Allah mtukufu: {Siku ambayo hayatafaa mali wala watoto} (Ash-shuaraa 88)

Naakasema Allah mtukufu {Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye . Na mamaye na babaye . Na mkewe na wanawe.kila mtu miongoni mwao siku hiyo atakuwa na hali itakayomtosha mwenyewe, (hana haja ya mwenziwe)} (Abasa aya 34-37)

## **TANO: kuamini hisabu na malipo**

Mwanadamu yatahesabiwa matendo yake kishaalipwe kulingana na matendo yake, asema Allah mtukufu: {Hakika marejeo yao ni kwetu . Kisha , bila shaka ,hisabu yao ni juu yetu.} (Al-ghashiyah aya 25:26.)

Asema Allah Mtukufu: {Afanyaye kitendo kizuri, atalipwa mfano wake mara kumi. na afanyaye kitendo kibaya hatalipwa ila sawa nacho tu (basi,kwa rehema ya Mwenyezi Mungu ). Nao (wote hao) hawatadhulumiwa.} (Al an-am 160)

Na akasema Allah Mtukufu: {Nasi tutaweka mizani za uadilifu siku ya kiama,na nafsi yoyote haitadhulumiwa hata kidogo.na hata kama likiwa(jambo hilo lina ) uzito mdogo wa chembe ya hardali nalo tutalileta;nasi tunatosha kuwa

wajuzi(wazuri kabisa)wa hesabu.} (Al-anbiyaa aya 47)

Na imepokewa na Ibn Umar (r.A.A) kutoka kwa mtume wa Allah "Hakika Allah atamsongelea muumin siku ya kiama amfunike kisha amuulize walikumbukaa dhambi lako Fulani aseme muumin ndio ya Allah Mola wangu mpaka akiyakiri madhambi yake akidhani ameshaangamia atasema Allah nimekusitiri duniani na leo nakusamehe kisha atapewa daftari lake la matendo mema , ama makafiri na wanafiki wataitwa mbele ya viumbe." {Hao ndio walimzulia Mola wao uwongo" sikizeni laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya madhalimu.} (Hud aya 18) (Mutafakun alyhi)

Na imeswihi kutoka kwa Mtume (S.A.W.) kwa hadith aliyo ipokeya kutoka kwa Mola wake mtukufu amesema: "Hakika Allah ameandika mema na mabaya kisha akayapambanua basi mwenye kuazimia kutenda jema kisha asilifanye Allah humuandikia jema kamili na anapo azimia kutenda jema kisha akalifanya Allah humuandikia mema kumi na humuungezea hadi elfu sabiin na mara nyingi zaidi , ma mwenye kuazimia kutenda baya moja kisha asilifanye Allah humuandikia jema kamili na anapo azimia baya kisha aklifanya Allah humuandikia baya moja" (Mutafakun alyhi)

Wameafikiana waislamu wote kuwepo kuhesabiwa na kulipwa kulingana na matendo, na jambo hili liniwafiki akili kwa sababu

Allah aliteremsha vitabu na akatuma mitume,na akafaradhishia watu kumuamini na kumtii yeye, kisha akakhofisha mwenye kuacha kumtii na kutomuamini na kutowatii mitume yake kwa adhabu kali na yenye kuumiza siku ya kiyama kama kusingekuwa na hisabu wala malipo yangalikuwa haya yote ni upuzi ambao Allah hasifiki kufanya jambo la ki puzi lisilokuwa na faida. Ameashiria Allah kwahilo aliposema : {Na kwa yakini tutawauliza wale waliopelekewa (mitume), na pia tutawauliza (Mitume) waliopelekwa. tena tutawaambia kwa ujuzi (uliokamili kila walilolitenda) wala hatukuwa mbali (nao walipokuwa wakifanya).} (Al-aaraf 6:7)

## **SABA:KUAMINI PEPO NA MOTO**

Kwamba ni marudio ya milele kwa viumbe , pepo ni nyumba ya neema alizoziandaa Allah kwa waumini wenye kumcha yeye, walioamini waliyofaradhishiwa na Allah na wakamtii Allah na Mtume wake kwa kumtakasia yeye peke yake ibada, wakimfuata Mtume wake, kuna aina za neema zote ambazo hakuna jicho lililowahi kuziona wala hakuna sikio lililowahi kuzisikia wala hakuna mtu aliyefikiria hizo neema. Asema Allah mtukufu: {Hakika wale walioamini na kutenda mema, basi hao ndio wema wa viumbe. Malipo yaokwa mola wao nimabustani ya daima ambayomito inapita mbele yake, wakae humo milele; Mwenyezi Mungu amewaridhia, nao wameridhika (malipo) hayo ni kwa yule anayemuogopa mola wake.} (Al-bayyinah 7:8)

Akasema tena Allah mtukufu: {Nafsi yoyote haijui waliyofichiwa katika hayo yanayofurahisha macho (huko peponi): ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyafanya.} (As-sajdah aya 17)

**Aliulizwa Hassan Basri mbonaa twaona mataabiin wanafanya ibada sana kuliko maswahaba, kwa jambo gani maswahaba waliwatangulia? akasema Hassan hawa wanafanya ibada lakini dunia iko moyoni mwao lakini maswahaba walifanya ibada ikiwa akhera iko moyoni mwao.**

Na neema bora zaidi kuliko zote nikumtazama Allah mtukufu huko peponi. Amesema Allah Mtukufu: {Nyuso (nyingine)siku hiyo zitangara (kweli kweli ),zinamtazama mola wao (au neema alizo wapa)} (Al-qiyama aya 22-23)





Amesema Allah Mtukufu. {Wale waliofanya wema watapata (jaza ya ) wema (wao) na zaidi} (Yunus 26)

Wema uliotajwa hapa ni pepo na zaidi iliotajwa hapa ni kumuangalia Allah Mkarimu kama alivyo sema Mtume (S.A.W) “watakapo ingia watu wa peponi peponi mwao atasema Allah mtukufu: je mwataka kitu chochote ni waongeze? watasema kwani hujazifanya nyuso zetu tiyari nyeupe kwani si umetuingiza tayari peponi na ukatuepusha na moto, akasema hapo ndipo itafunguliwa pazia, (na wamuone Allah) basi hakuna kitu bora walichokitaka kama kumuona Allah mtukufu kisha akasoma Mtume (S.A.W) aya hii: {Wale walifanya wema watapata (jaza ya) wema (wao)na zaidi} (Yunus 26) (Imepokewa na Muslim)

Ama moto ni nyumba ya adabu aliyoandaa Allah Mtukufu kwa makafiri na wanafiki madhalimu waliomkufuru yeye na wakawakanusha Mitume, ndani humo mna aina zote adabu na majonzi wasiyoweza kufikiriwa. Asema Allah Mtukufu: {Na ogopeni moto ambao umewekewa wenye kukanusha amri za mwenyezi mungu } (Aali imran aya 131)

Akasema tena {Hakika tumewaandalia (tumewawekea tayari) madhalimu moto ambao kuta zake zitawazunguka. na wakiomba msaada (kwa kiu kubwa iliyowashika) watasaidiwa kwa kupewa maji kama shaba iliyoyayushwa itakayoziunguza nyuso zao. Kinywaji kibaya kilioje hicho. Na mahali pabaya palioje.} (Al kahf aya 29)

Asema allah mtukufu: {Kwahakika Mwenyezi Mungu amewalaani makafiri na amewaandalia moto unaowaka kwelikweli. watakaa humo daima; hawatapata kipenzi wala msaidizi. siku ambayo nyuso zao zitapinduliwa pinduliwa (zitaponguzwa) motoni, waseme:” laiti tungemtii mwenyezi mungu na tunge mtii mtume.} (Al-ahzab aya 64-66)

Yule ambaye atapata adhabu duni zaidi, Allah atuepushe ni kama alivyo msifia mtume (S.A.W): “hakika mtu atakaye kuwa na adabu duni motoni siku ya kiama, ni mtu ambaye ataekewa kaa la moto katika nyayo yake lakini ubongo wake utachemka. (Imepokewa na Bukhari)

## MATUNDA YA KUAMINI SIKU YA MWISHO

1. Ni kuhakikisha nguzo moja katika nguzo za imani kwasababu kumuamini Allah hakuwi sawa paka mtu aamini siku ya mwisho kwahiyo ni miongoni mwa nguzo za imani ndio maana Allah alitufaradhisia sisi kumpiga asiyeamini hiyo siku ya mwisho. Akasema Allah mtukufu: {Piganani na wale wasiomuamini mwenyezi mungu wala siku ya mwisho} (At tawba 29)
2. Kupata utulivu duniani na akhera na ahadi ya malipo makubwa ,asema Allah mtukufu: {Sikizeni vipenzi vya Mwenyezi Mungu hawatakuwa na khofu (siku ya kiyama)wala hawatahuzunika} (Yunus 62)
3. Ahadi ya malipo makubwa, asema Allah Mtukufu: {Katika walioamini (mitume ya zamani huko) na mayahudi na wakristo na wasabai; yoyote (miongoni mwao) atakayemwamini mwenyezi mungu (sasa kama anavyosema nabii muhammad)na akaamini siku ya mwisho na akafanya vitendo vizuri,basi watapata thawabu zao kwa Mola wao, wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika} (Al baqarah 62)
4. Kuhimiza katika kufanya vitendo vizuri, asema Allah mtukufu: {Enyi mliaoamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini mtume na wenye mamlaka juu yenu, walio katika nyie (waislamu wenzenu) . Na kama mkikhitalifiana juu ya jambo lolote basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho hiyo ndio kheri , nayo ina matokeo bora kabisa.} (An nisaa aya 59)

Na akasema Allah Mtukufu: {Wanaoimarisha misikiti ya Mwenyezi Mungu ni wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho} (At tawba 18)

Na asema Allah Mtukufu: {Bila shaka mnao mfano mwema (ruwaza nzuri) kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa mwenye kumuogopa mwenyezi mungu na siku ya mwisho, na kumtaja Mwenyezi Mungu sana.} (Al-ahzab 21)

Na akasema Allah Mtukufu {Kwa yakini umekuwa mfano mzuri kwenu katika mwendo wao, kwa amuogopaye Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho.} (Al-mumtahinah 6)

Asema Allah {Na simamisheni ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hivyo ndivyo anavyoagizwa Yule anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho.} (At-talaq 2)

5. Anakataza kutenda vitendo vibaya: amesema Allah mtukufu: {Wala haiwajuzii kuficha (mimba) aliyoumba Mwenyezi Mungu katika matumbo yao, ikiwa wanamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho.} (Al-baqarah 228)

Na asema Allah mtukufu: {Na mtakapowapa wanawake talaka, (ya kwanza au ya pili); nao wakamaliza eda yao, basi (nyinyi jamaa wa mke) msiwazuie kuolewa ( au kurejewa) na waume zao endapo baina yao wamepatana. Hayo anaonywa nayo yule miongoni mwenu anayemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho.} (Al-baqarah 232)

Amesema Allah mtukufu: {Hawatakuomba ruhusa wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho.(hawatakutaka ruhusa) kutoipigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafasi zao. Na Mwenyezi Mungu anawajua wanaomcha. Wanakuomba ruhusa wale wasiomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na nyoyo zao zina shaka; kwa hiyo wanasitasita kwa ajili ya shaka yao.} (At tawba : 44, 45)

Kwahio asiyeamini siku hii hajichungi na kufanya yaliyo haramishwa, wala haoni haya kwa Allah. {Je umemuona (unamjua) yule anayekadhibisha dini, (asiyeamini malipo ya akhera)? Huyu ni yule anayemsukuma yatima. Wala hajihimiza kuwalisha maskini (wala hawahimiza wenziwe)} (Maun 1:3)

6. Kuwaliwaza waumini kwa yanayo mpita hapa duniani kwa neema na thawabu anazo zitarajia kesho akhera, kwani pepo ndio kufaulu kukubwa na hayawi maisha ya dunia ila starehe zenye kudanganya. Asema Allah Mtukufu: {Kila nafsi itaonja mauti. Na bila shaka mtapewa ujira wenu kamili siku ya kiyama. Na aliyewekwa mbali na moto na akaingizwa peponi, basi amefuzu (amefaulu kweli kweli). Namaisha ya

**Amesema Ummul M u u m i n i n a 'Aisha (r.a) kwa mwanamke: "Zidisha k u y a k u m b u k a mauti moyo wako utalainika."**

dunia (hii) si kitu ila ni starehe idanganyayo (watu)} (Aa-li imran 185)

Amesema Allah mtukufu {Sema : " mimi naogopa adhabu ya siku kubwa (hiyo) ikiwa nitamuasi mola wangu." Atakaye epushwa nayo (adhabu hiyo) siku hiyo (ya kiyama), bila shaka amemrehemu ( mwenyezi mungu); na huku ndiko kufaulu kuliko dhahiri." (Al an-am : 15:16)

Na akasema Allah mtukufu: { Hali ya kuwa ya akhera ni bora (zaidi kabisa) na yenye kudumu.} (Al-alaa : 14)

Kumliwaza muumini kwa yale yanampita duniani. Kwa zile neema na thawabu anazo zisubiri muumin, kwa hiyo pepo ni kufaulu kukubwa sana, na hayakuwa maisha yaa duniani ila starehe yenyekuhadaa. Asema Allah Mtukufu. {Kila nafsi itaonja mauti. Na bila ya shaka mtapewa ujira wenu kaamili Siku ya Kiyama. Na atakaye epushwa na Moto na akatiwa Peponi basi huyo amefuzu. Na maisha ya dunia si kitu ila ni starehe ya udanganyifu.} (Aa-li imran 185)

Asema Allah Mtukufu {Sema : " mimi naogopa adhabu ya siku kubwa (hiyo) ikiwa nitamuasi mola wangu." Atakaye epushwa nayo (adhabu hiyo) siku hiyo (ya kiyama), bila shaka amemrehemu ( Mwenyezi mungu); na huku ndiko kufaulu kuliko dhahiri} (Al an-am : 15:16)

Asema Allah Mtukufu { Hali ya kuwa ya akhera ni bora (zaidi kabisa) na yenye kudumu.} (Al-alaa : 14)

**Amesema Alhasan (R.A):" mwenye kuyatambua mauti yanakuwa masaibu ya dunia yote kwake dhalili.**

**Moyo hauwi sawa wala hautengei, wala haupati raha wala hautulii na kupata utulivu ila kwa kumuabudu Mola wake na kumpenda na kurudi kwake.**

**Sheikh Al islam**



## Marejeo

1. Eleza uhusiano baina ya dini na imani kwa kutulia na kupata raha.
2. Eleza nini imani, na taja athari zake kwa jamii ?
3. Ni vipi vyenye kuambatana na kumuamini Allah Mtukufu?
4. Niipi amali bora zaidi tena tukufu mbele ya Allah ?
5. Taja unavyovihisi kutokana na matunda ya kumuamini Allah kwako na kwa familia yako na hadi kwa mujtamaa wote.
6. Ni vipi vinavyoambatana na kuamini mitume?
7. Kwanini ilikuwa miongoni mwa kuamini Mtume (S.A.W) kwa maswahaba ni kumpenda pia?
8. Elezea matukio ya kiyama kwa uataratibu wake unaoufahamu kuanzia kwa ishara zake ndogo mpaka watakapoingia peponi watu wa peponi, na kuingia motoni watu wa motoni.
9. Ni amali gani muhimu inayomuingiza mja sana peponi na kumuokoa mja kutokana na moto?
10. Eleza matunda ya kuamini kwako siku ya mwisho katika ibada zako na uchaji Mungu wako.
11. Ni ipi neema kubwa peponi? Na ni ipi adhabu ya chini kabisa motoni?